



## Atakayesema: Sub-haanallaahi wabihamdi, (Ametakasika Mwenyezi Mungu Mtukufu na sifa njema ni zake) ataoteshewa mti wa mtende peponi

Imepokelewa kutoka kwa Jabiri -radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -  
rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Atakayesema: Sub-haanallaahi wabihamdi,  
(Ametakasika Mwenyezi Mungu Mtukufu na sifa njema ni zake) ataoteshewa mti wa  
mtende peponi".

[Sahihi] [Imepokelewa na Imamu Tirmidhiy]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake yakuwa atakayesema: "Ametakasika  
Mwenyezi Mungu" ninamtakasa "Mtukufu" kwa dhati yake na sifa zake na vitendo vyake "na  
sifa njema ni zake" zikiwa zimeambatanishwa na kugemeza sifa za ukamilifu wake Mtukufu;  
atasimikiwa na kupandiwa mti wa mtende katika ardhi ya Pepo kwa kila mara atakayosema.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/4201>

